

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE

01

KISWAHILI

Muda: Saa 1:30

MAJIBU

Mwaka: 2018

Maelekezo

1. Mtihani huu una sehemu A, B, C, D na E zenye jumla ya maswali **matano (5)**
2. Jibu maswali **yote**.
3. Andika majibu yote kwenye nafasi zilizoachwa wazi katika kila swali.
4. Andika majibu yote kwa kutumia kalamu ya wino wa **bluu** au **mweusi**

maktaba.tetea.org



SEHEMU A: (Alama 10)

1. Sikiliza kwa makini sentensi zinazosomwa kisha uziandike kwa usahihi katika nafasi zilizoachwa wazi
- (i) Baba ni fundi seremala.
 - (ii) Kila asubuhi ninakunywa uji.
 - (iii) Mwalimu wetu ni mshereheshaji.
 - (iv) Bustani yetu imepandwa maua.
 - (v) Mgeni ameporwa mali zake.

SEHEMU B (Alama 10)

2. Andika umoja na wingi wa sentensi zifuatazo; kipengele cha (i) kimetumika kama mfano.

(i) Umoja: Kiti chake kimevunjika.

Wingi: Viti vyake vimevunjika.

(ii) Umoja: Hiki ni kitabu changu.

Wingi: **Hivi ni vitabu vyangu.**

(iii) Umoja: Kiatu changu cheupe kimepotea.

Wingi: **Viatu vyangu vyeupe vimepotea.**

(iv) Umoja: **Mpishi amepika chakula kitamu.**

Wingi: Wapishi wamepika chakula kitamu.

(v) Umoja: Kalamu yako ilipotea darasani.

Wingi: **Kalamu zako zilipotea darasani.**

(vi) Umoja: **Mti huu ulianguka juzi.**

Wingi: Miti hii ilianguka juzi.

SEHEMU C (Alama 10)

3. (a) Kamilisha methali ulizopewa kwa kuandika jibu sahihi katika nafasi zilizoachwa wazi.

(i) Fahali wawili

Methali kamili ni **Fahali wawili hawakai zizi moja.**

(ii) Mvumilivu,

Methali kamili ni **Mvumilivu hula mbivu.**

(b) Toa maana ya methali zifuatazo kwa kuandika jibu sahihi katika nafasi zilizoachwa wazi:

(i) Kidole kimoja hakivunji chawa

Maana yake ni **ushirikiano ni muhimu, mtu mmoja hawezi kufanikiwa peke yake.**

(ii) Ahadi ni deni

Maana yake ni **ukiahidi jambo ni lazima ulitimiza.**

(c) Nahau “tia doa” ina maana gani?

Nahau “tia doa” ina maana ya **kuharibu sifa au heshima ya mtu au jambo.**

SEHEMU D (Alama 10)

4. Weka alama za uandishi katika sentensi zifuatazo kwa kuandika alama sahihi katika nafasi iliyoachwa wazi.

(i) Je utafika saa ngapi

Je, utafika saa ngapi?

(ii) Embe nanasi na papai ni matunda

Embe, nanasi na papai ni matunda.

(iii) Loo kwani wewe ni nani

Loo! Kwani wewe ni nani?

(iv) Oyee nani amefunga goli

Oyee! Nani amefunga goli?

(v) Haba na haba hujaza kibaba

Haba na haba hujaza kibaba.

SEHEMU E (Alama 10)

5. Soma kwa makini shairi lifuatalo kisha jibu maswali yanayofuata kwa kuandika jibu lililo sahihi katika nafasi iliyoachwa wazi.

Nchi yangu naipenda, hakika nawaeleza,

Ni nchi yenye matunda, huwezi kuyamaliza,

Na asali tunapenda, nchi yajitokeza,

Tanzania Tanzania, nchi yangu nakupenda.

Kuna mrefu mlima, Kilimanjaro twakwea,

Ardhi ya wakulima, rutuba imeenea,

Pia mbuga za wanyama, Mikumi nawaambia,
Tanzania Tanzania, nchi yangu nakupenda.
Tamati ninaishia, mengi nimewaeleza,
Kabla sijaishia, mito ninawaeleza,
Bahari pia sikia, na maziwa yapendeza,
Tanzania Tanzania, nchi yangu nakupenda.

Maswali:

a) Nini maana ya neno “tamati” kama lilivyotumika katika ubeti wa tatu?
Maana ya “tamati” ni **mwisho au hitimisho**.

b) Shairi hili linahusu nini?

Shairi hili linahusu **kuipenda na kuisifu nchi ya Tanzania**.

c) Taja mlima mrefu uliotajwa na mshairi.

Mlima uliotajwa ni **Mlima Kilimanjaro**.

d) Taja mbuga ya wanyama iliyotajwa katika shairi.

Mbuga iliyotajwa ni **Mikumi**.

e) Taja vyanzo viwili vya maji vilivyotajwa katika shairi hili.

Chanzo cha kwanza ni **bahari**.

Chanzo cha pili ni **maziwa**.